**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:

   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

---

***Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua kiteuzi kifaacho zaidi.***

Atyang ni____1____ anayesomea shule ya ____2____ ya Malaba. Ina ____3____ hadi darasa la nane. ____4____ yuko katika darasa____5____ tano. Msichana huyu ni mpole na ____6____ tabia bora. Ni rafiki ya kila mtu awe mtoto au mtu mzima.

Tabia ____7____ nzuri humwezesha kupendwa na ____8____ na wanafunzi wenzake. Licha ya ____9____ na tabia ____10____ kupendeza, Yeye ndiye mfano mwema wa wanafunzi wenye nidhamu ya hali ya juu. Yeye pia huongoza darasani wakati wa matokeo ya ____11____. Hutuzwa zawadi ____12____, wazee husema ukiviona vyaelea vimeundwa. Mtoto____13____ hapotezi wakait wake ovyo ovyo. Yeye na vitabu ni kama ulimi na mate. Huwa na biddi ya ____14____ ajengaye____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mwanafunzi | B. mhadhiri | C.mzembe | D. watoto |
| 2. | A.sekondari | B.mzingi | C.msingi | D.skuli |
| 3. | A.chekezea | B.chekechea | C.chekeshea | D.chekesha |
| 4. | A.Wewe | B.Yeye | C.Huu | D.Mwenye |
| 5. | A.ya | B.za | C.la | D.kwa |
| 6. | A.yenye | B.mwenye | C.chenye | D.zenye |
| 7. | A.yake | B.zake | C.chake | D.lake |
| 8. | A.kweshimiwa | B.kwaheshima | C.kuaeshimiwa | D.kuheshimiwa |
| 9. | A.kuwa | B.kua | C.kuuwa | D.kugwa |
| 10. | A.cha | B.la | C.ya | D.zake |
| 11. | A.mtihaani | B.mutihani | C.mtiani | D.mtihani |
| 12. | A.zingi | B.nyingi | C.mengi | D.mingi |
| 13. | A.njema | B.muema | C.mwema | D.chema |
| 14. | A.mdudu | B.mchwa | C.kuwa | D.muchwa |
| 15. | A.kisugugi | B. chungu | C.nyumba | D.kichuguu |

*Kuanzia swali la 16-30, kulingana na maagizo*

16. Kanusha sentensi hii

*Kaka aliweza kuliinua shoka*

A. Kaka hakuweza kuliinua shoka
B. Kaka hawezi kuliinua shoka
C. Kaka haezi kuiiinua shoka
D. Kaka anaeza kuliinua shoka

17. Kamilisha mehtali hii

*Haraka haraka haina*

A. amani B. maana
C. baraka D. faida

18. *Andika tarakimu hii kwa maneno: 9009*

A. Elfu tisa na tisa
B. Elfu mia tisa na tisa
C. Mia tisa elfu na tisa
D. Mia tisa na tisa

19. Umbo hili ni



A. wimbi B. zigizagi
C. mche D. pia

20. Neno mtoto liko kaitka ngeli gani?

A. KI - VI B. LI - YA
C. A - WA D. I - ZI

21. Anayepokea nauli kwenye gari anaitwa

A. abiria B. mhazili
C. hamali D. utingo

22. Tumia kiulizi kifaacho

*Ni kijana _____ aliyeitika?*

A. mgani B. yupi
C. wapi D. gani

23. Mlinzi wa lango kuu shuleni huitwa

A. bawabu B. askari
C. bawaba D. komeo

24. Kikembe cha kuku ni

A. kinda B. kiyoyo
C. kifaranga D. kimeme

25. Tegua kitendawili kifuatacho

*Ajenga lakini hana mikono*

A. samaki B. kuku
C. nungunungu D. nyuki

26. Nitamwitaje mwanawe kaka yangu?

A. Ami B. Mpwa
C. Umbu D. Shemeji

27. Tulikula wali_______nyama.

A. na B. pia
C. kwa D. tena

28. Tumia eneywe kwa ufasaha

*Vazi ______ni chafu.*

A. lenyewe B. yenyewe
C. mwenyewe D. enyewe

29. Kamilisha tashbihi hii

*Chakula hiki ni kitamu kama*

A. shubiri B. sukari
C. lawalawa D. halua

30. Jiko ambalo hutumia makaa huitwa

A. Bilauri B. Seredani
C. Kanga D. Fahali

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 - 40.*

Malaria ni ugonjwa unaoletwa na mbu. Mbu hupenda kuishi mahali penye giza ili wasionekane na kuangamizwa na binadamu. Hujitokeza wakati wa magharibi kuwashambulia watu. Wao hutagia kwenye takataka au maji yaliyokwama. Mikebe mitupu yafaa kuharibiwa ili isiwe makazi ya mbu.

Dalili za ugonjwa wa homa ya malaria ni; kuwangwa na kichwa,tumbo au mgongo, kuwa mlegevu, kupoteza hamu ya chakula na wakati mwingine kutapika.

Ni muhimu kuishi katika mazingira safi ili kujikinga na malaria. Hakikisha kuwa unalala ndani ya chandarua kisichopitisha mbu; kilichotiwa dawa ya kufukuza mbu. Maji yaliyotuama sharti yaondolewe na nyasi zilizo karibu na maskani ya waja kukatwa. Wanaoishi kwenye maeneo yenye mbu wanaweza kumeza tembe za kuzuia homa ya malaria.

Malaria huua! Yapasa tushirikiane ili kuangamiza ugonjwa huu.

---

**31.** Maradhi ya malaria husababishwa na

A. mbungo B. mbu

C. konokono D. nzi

**32.** Jina jingine la malaria ni

A. homa ya mapafu

B. malale

C. homa ya matumbo

D. homa ya mbu

**33.** Mbu huishi mahali penye giza ili

A. wasionekane na binadamu

B. wasionekane na kuangamizwa na binadamu

C. wafurahie chakula

D. wapate nafsi ya kulala

**34.** Mbu hushambulia watu wakati gani?

A. Mashariki B. Mapambazuko

C. Magharibi D. Alasiri

**35.** Maji yaliyokwama ni

A. maji yaendayo kwa kasi

B. maji baridi

C. maji moto

D. maji yaliyokusanyika bila kusonga

**36.** Mikebe mitupu huharibiwa ili

A. mbu wapate nafasi ya kutagia

B. mbu wakose nafasi ya kutagia

C. mbu wawe safi

D. mbu wasipate majeraha

**37.** Ni ipi si dalili ya malaria?

A. Kuwangwa na kichwa

B. kuumwa na tumbo au mgongo

C. kuwa mlegevu

D. kuwa na hamu ya chakula

**38.** Unajikinga na malaria kwa

A. kulala ndani ya chandarua

B. kulala nje ya chandarua

C. kutolala ndani ya chandarua

D. kulala karibu na chandarua

**39.** Neno lenye maana sawa na magonjwa ni

A. mawaidha B. maradhi

C. radi D. ratiba

**40.** Mwishoni mwa kifungu mwandishi anatushauri

A. Tishirikiane ili kuangamiza binadamu

B. Tushirikiane tuangamize mikebe

C. Tushirikiane tuangamize malaria

D. Tushirikiane tucheze pamoja

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.**

Nyani hupenda kuishi katika vikundi. Kikundi huweza kuwa na nyani zaidi ya mia moja. Wakati wa usiku nyani hujificha porini kwenye vilele vya miti mirefu. Nyani huweza kumhepa adui kwa kuchupa kutoka kitanzu kimoja cha miti hadi kingine.

Asubuhi huteremka chini kutafuta chakula. Chakula cha nyani ni wadudu, matunda, mahindi muhogo na vyakula vingine vinavyopandwa mashambani. Nyani pia hukamata na kula kuku na mabata. Kundi la nyani laweza kulivamia shamba na kusababisha hasara kubwa kwa mkulima.

Adui mkubwa wa nyuni ni chui. Chui hupenda kula nyama ya nyani. Silaha kubwa ya nyani ni meno yake. Nyani ana meno makali sana. Kundi moja la nyani laweza kumshambulia chui na kumraruararua kwa meno mpaka wakamwua.

41. Ni mnyama yupi huepnda kuishi kwa vikundi
A. chui
B. binadamu
C. nyani
D. paka

42. Kikundi kimoja kinaweza kuwa na
A. Chui zaidi ya mia moja
B. Nyani chini ya mia moja
C. Chui mia moja
D. Zaidi ya nyani mia moja

43. Vilele vya miti mirefu ni makao ya
A. porini
B. nyani
C. chui
D. wadudu

44. Kuchupa kutoka kitanzu kimoja hadi kingine ni hali ya
A. kuhepa adui
B. nyani kustarehe
C. kutafuta chakula
D. kujifundisha kuruka

45. Kati ya hivi vyakula ni kipi si chakula cha nyani
A. Kuku
B. Bata
C. Chui
D. Matunda

46. ______hupata hasara kutokana na nyani
A. Chui
B. Mkulima
C. Kuku
D. Matunda

47. Adui mkubwa wa nyani ni
A. Mkulima
B. Mwalimu
C. Chui
D. Bata

48. Chui anaweza kuaga kutokana na
A. meno ya nyani
B. njaa
C. hasara ya mkulima
D. mawindo haba

49. Makao ya nyani ni
A. pangoni
B. shambani
C. porini
D. zizini

50. Kichwa sahihi cha habari hii ni
A. Safari ndefu
B. Mnyama nimpendaye
C. Sherehe
D. Nyani